

## **Maswali**

1. Huyu mtu alisafiri kwenda wapi?
2. Nani alimuumiza?
3. Kuhani alikuwa mwema?
4. Mlawi alikuwa mwema?
5. Msamaria alikuwa mwema?
6. Msamaria alimsaidia?
7. Msamaria alimpeleka huyo mtu wapi?
8. Msamaria alimpa mtunza nyumba ya wageni nini?
9. Yesu aliuliza swalii gani?
10. Lazima tuwe wema kwa nani?

## **Majibu**

1. Huyu mtu alikuwa akisafiri kwenda Yeriko
2. Wezi walimuumiza.
3. Kuhani hakukuwa mwema.
4. Mlawi hakukuwa mwema.
5. Msamaria alikuwa mwema.
6. Alimuosha na kumfunga vidonda kwa utambaa.
7. Alimpeleka kwa nyumba ya wageni.
8. Alimpa mtunza nyumba ya wageni dinari mbili ya kumtunza.
9. Yesu aliuliza, "Ni mtu yupi aliyemhurumia yule mtu aliyekuwa amejeruhiwa."
10. Lazima tuwe wema kila mtu.

## **SHULE YA JUMAPILI YA CBM**



**Awamu ya 1 Mwaka wa 1**

# **41 Msamaria Mwema**

## **Marejeo**

Luka 10:30-37

## **Kiini cha somo**

Kuwa mwema kwa kila mtu

## **Maneno maalum**

1. Yerusalem + Yeriko + chini + mtu anasafiri
2. Wezi + umiza + nyang'anya
3. Moto + kuhani + hakuna usaiadizi
4. Moto + mlawi + hakuna usaidizi
5. Msamaria + saidia + funga utambaa + punda
6. Nyumba ya wageni + dinari mbili + mtu yupi mwema?


**41.1** Somo hili ni mfano mwingine aliousema Yesu. Alikuwa aktuonyesha kuwa tusaidie na kumtendea mema mtu yejote mwenye shida kwamba ni mtu tunayempenda au la.

Palikuwa na mtu aliyejekuwa anasafiri akitoka Yerusalem, mji mkuu akielekea mji wa Yeriko, uliokuwa chini bondeni penye kijani kibichi karibu na mto Yordani. Mtu huyu alikuwa na haraka ili afike Yeriko kwa hiyo aliondoka alfajiri na mapema akiwa peke yake.

Na kadiri alivyokuwa akisafiri ndivyo njia ile mtelemko wake mkali ulivyo zidi kuongezeka na barabara ilipita katikati ya miamba mwili iliyoinuka juu. Kulikuwa na miamba mikubwa sana iliyoshikamana pande zote mbili. Mtu huyu akafanya haraka ili kupita eneo hili lililokuwa ni la hatari sana.

**41.2** Na kisha akasikia nyayo za mtu anayetembea akiya nyuma yake. Akageuka atazame nyuma, lakini mikono ya watu katili ikamshika na kumwangusha chini na kisha wakamvuta na kumweka kando ya njia. Alijikuta akiwa amezungukwa na wanyang'anyi. Walimwibia mfuko wenyepesa, wakamvua nguo, wakakimbia wakimwacha akiwa anavuja damu mwili mzima na alikuwa amezimia. Yule mtu akajaribu kuinuka, lakini akashindwa maana alikuwa ameumizwa sana na akawa hana nguvu kabisa. Jua likimuwakia, likinguza mwili wa maskini huyu!

**41.3** Alilala pale masaa yote akifikiria kama kweli atakuja mtu amsaidie. Hatimaye, akasikia kishindo cha nyayo. Kuna mtu anakuja. Huyu alikuwa ni kuhani. Kwa kweli mtu huyu alipaswa kumsaidia kabisa. Lakini kuhani akapita kando tena akapitia upande wa pili wa barabara. Yule mtu akajaribu amwite yule kuhani, lakini alishindwa. Kwa kuwa ulimi wake ulikuwa umekwisha kukauka na tena ulikuwa umevimba.



**41.4** Muda baada ya muda ukawa-unapita tu. Yule mtu hali yake ikawa inaendelea kuwa mbaya zaidi. Na tena akasikia kishindo cha nyayo. Kishindo cha yule mtu kikawa kimemkaribia. Yule mtu aliyejeruhiwa akatazama, akamwona Mlawi akipita kando. Yule mtu akakoroma, lakini Mlawi akavuka na kupita upande wa pili na akaenda zake.

**41.5** Yule mtu akawa amelala pale kwa muda mrefu sana. Ikawa sasa inakaribia kuingia giza. Mara hii tena akasikia kishindo cha nyayo. Yule mtu hakutazama tena maana alikuwa amekwisha kukata tamaa ya kupata msaada. Kisha akahisi mikono ya huruma ikimwinua. Kwa mshangao alipofungua macho yake alimwona mtu ambaye ni mgeni-Msamaria. Yule mtu akampaka mafuta na divai majeraha na akamfunga kwa utambaa majeraha yake taratibu.



Msamaria alitumia nguo yake kufunga majeraha ya yule mtu na akamnyanya na kumweka juu ya punda wake. Wakatembea polepole kwenye barabara. Msamaria hakuwa amepanda punda tena, kwa kuwa yule mtu alikuwa mahututi asingeweza kukaa peke yake pasipo kushikwa na mtu, hivyo msamaria alikuwa akitembea huku mikono yake imemshikilia. Walipofika nyumba ya wageni, Msamaria alimwita mtunzaji wa nyumba ya wageni aje kumsaidia. Ndipo walipomnyanya yule mtu na kumlaza kitandani.

**41.6** Msamaria alikesha usiku wote akimhudumia. Na asubuhi akamwita mtunza nyumba ya wageni, "Inanipasa niendelee na safari yangu, akamwambia; chukua hizi dinari mbili, naomba umtunze huyu. Na chochote utakachogaramika zaidi, mimi nitakaporudi nitakulipa."

Yesu akauliza, "**Ni mtu yupi aliymhurumia yule mtu aliyejekuwa amejeruhiwa?**"

